TANGAZO LA SERIKALI Na. 148 la tarehe 3/3/2023

SHERIA YA MIPANGO MIJI
(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetolewa Chini ya Kifungu cha 8(1) na 23(1))*

AMRI YA KURASIMISHA MAKAZI YASIYOPANGWA ENEO LA NATOTO YA MWAKA 2023

Jina

1. Amri hii itaitwa Amri ya Kurasimisha Makazi yasiyopangwa Eneo la Natoto ya Mwaka 2023.

Kutangaza Eneo la upangaji Sura ya 355

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji (mpango wa urasimishaji) kwa madhumuni ya Sheria ya Mipango Miji.

Mpango katika eneo la kwenye Jedwali

3. Mipango ya jumla na kina ya eneo lililoainishwa kwenye Jedwali itaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipango Miji na Mkurugenzi wa Mji wa Nanyamba.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la upangaji lipo ndani ya mipaka ifuatayo:-

"Mpaka unaanzia kwenye kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba N1 yenye majira - nukta 587375MS, 8818432KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Magharibi kwa kufuata barabara ya Newala - Mtwara kwa umbali wa kilomita 0.5 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba N2 yenye majira - nukta 587025MS, 8818168KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Mashariki katika uelekeo wa $81^0$ 29'57'' kwa umbali wa kilomita 0.7 hadi katika bonde la mto Dinyecha hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba N3 yenye majira - nukta 586098MS, 8818663KZ; baada ya hapo mpaka unafuata mwelekeo wa mto Dinyecha hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba N4 yenye majira - nukta 586457MS, 8817654KZ; baada ya hapo mpaka unafuata mto Natoto hadi makutano ya barabara ya Namkuku- Nanyamba kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba N5 yenye majira - nukta 587736MS, 8817632KZ; baada ya hapo mpaka unafuata barabara ya Namkuku - Nanyamba hadi ulipoanzia."

Dodoma
6 Februari, 2023

ANGELINE S. MABULA,
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na,*
*Maendeleo ya Makazi*